

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TISA

KIKAO CHA KWANZA

08 APRILI, 2025



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TISA

KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 08 APRILI, 2025

I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:

II. DUA:

III. TAARIFA YA SPIKA:

IV. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

V. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

1. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Mlowo – Isansa - Magamba hadi Mkwajuni Wilayani Songwe.

2. MHESHIMIWA BALOZI LIBERATA RUTAGERUKA MULAMULA (KUTEULIWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Zahanati Kitongoji cha Kakoni - Misenyi ili iweze kuhudumia Wananchi wa Kitongoji hicho na jirani.

3. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini fedha za ujenzi wa Majengo ya *X-ray*, *OPD*, *Wodi*, *Mortuary*, Kuchomea Taka, kufulia na *Walk ways* zitapelekwa Vituo vya Afya vya Kondoa.

4. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itavipatia Magari ya kubebea Wagonjwa Vituo vya Afya vya Magazini na Lusewa - Namtumbo.

5. MHESHIMIWA JOSEPH ANANIA TADAYO (MWANGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Zahanati iliyoboreshwa ya Mangio iliyopo Kata ya Mwaniko Wilayani Mwanga.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

6. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mpango gani wa njia mbadala ya kukuza uchumi wa Wananchi wa Hai kutokana na uhaba wa ardhi ya uzalishaji.

WIZARA YA NISHATI:

7. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini umeme utapelekwa katika eneo la Kitame Kata ya Makurunge ili kuwasaidia wazalishaji wa chumvi.

WIZARA YA KILIMO:

8. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa Miradi ya Umwagiliaji ya Udima na Mbwasa - Manyoni.

WIZARA YA MAJI:

9. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itajenga Mradi wa Maji Kata ya Matemanga katika Vijiji vya Milonde, Matemanga na Changarawe – Tunduru.

10. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Wananchi wa Kijiji cha Sambaru Kata ya Mang'onyi Singida Mashariki watapata maji safi na salama.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

11. MHESHIMIWA SAADA MANSOUR HUSSEIN (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itamaliza changamoto ya Vituo vya Polisi na vitendea kazi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

WIZARA YA AFYA:

12. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama ya matibabu ya kusafisha Figo katika Hospitali zetu nchini.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

13. MHESHIMIWA TOUFIQ SALIM TURKY (MPENDAE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha ongezeko la Vyombo vya Habari mtandaoni haliathiri maadili na utamaduni wa Taifa letu.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

14. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itaona haja ya kuwa na Kiwanda cha Asali Tarafa ya Kiwele - Sikonge.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

15. MHESHIMIWA DKT. PAULINA DANIEL NAHATO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza uhaba wa Mabweni katika Vyuo Vikuu vya Umma.

DODOMA
08 APRILI, 2025

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE

